JUU, kutoka kwa Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi katika maharafu ya ...
**PICHA: MPIGA PICHA WETU**

NIPASHE UK 5

# Majaliwa amulika mikoa yenye migogoro kutokana na mifugo

**Na Mwandishi Wetu,**
MOROGORO

*WAZIRI Mkuu, Kassimu Majaliwa ameitaja mikoa ya* Morogoro, Iringa, Pwani, Lindi, Arusha, Manyara, Kagera, Katavi, Tabora, Tanga na Mwanza kuongoza katika shida za kijamii na kimazingira zinazosababishwa na mifugo.

Amesema mikoa 11 hiyo inakabiliwa na changamoto nyingi zinazosababishwa na mifugo ikiwamo migogoro ya wakulima na wafugaji, uharibifu wa vyanzo vya maji na misitu iliyohifadhiwa kisheria.

Katika kikao kazi cha viongozi mkoani Morogoro jana, Majaliwa alisema kikao hicho kinachotokana na maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan yanahusu kusimamia kwa karibu sekta ya mifugo ili kutatua kero zilizopo.

"Leo (jana) tunaona changamoto kubwa za wakulima na wafugaji zinazosababisha mauaji, wanakatana mapanga, hata jana (juzi) niliangalia kwenye runinga, nikaona kuna mahali wakulima wanalalamika mifugo imeingia kwenye mashamba yao ya mpunga na kuharibu mazao," alisema.

Majaliwa alisema kutokana na hali hiyo, kila kiongozi anapaswa kuwajibika kwa kusimamia haki, usalama na kutoa elimu elimu kwa jamii ambayo kwa sasa imekuwa na roho ya kikatili.

Majaliwa alisema kutokana na migogoro hiyo ya wakulima na wafugaji, jamii imekuwa na chuki, pia kumekuwa na vitendo vya rushwa miongoni mwa viongozi ambao pia wamekuwa wakichochea migogoro hiyo.

"Polisi wenyewe sasa hivi wameanza kudhibitiwa na wananchi, juzi juzi tu huko Malinyi ama Ulanga, polisi walifungiwa ndani ya nyumba chini ya udhibiti wa wananchi, tukifika hapo hiyo haina tija. "Chombo cha ulinzi na usalama kinadhibitiwa na raia, nini maana ya kuwapo kwake? Kwanini imetokea hiyo? Wananchi wamechoka au sisi viongozi hatuwajibiki?" Majaliwa alihoji.

Alisema Mkuu wa Nchi anapoonyesha kutoridhishwa na maeneo fulani, ni wajibu wa viongozi hao kuweka mpango mkakati wa pamoja wa kudhibiti changamoto za mifugo na kujua nini cha kufanya katika kukabiliana na changamoto hiyo.

Awali akitoa salamu za mkoa, Mkuu wa mkoa wa Morogoro, Fatuma Mwasa alisema kuwa yeye pamoja na viongozi wenzake wako tayari kupokea na kutekeleza maagizo na maelekezo yote yatakayotolewa na Waziri Mkuu na serikali kwa ujumla.

Alisema ujio wa Waziri Mkuu umeleta faraja kwa viongozi na wananchi wa Mkoa wa Morogoro.

Kikao hicho kiliwahusisha Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Fatuma Mwasa, wakuu wa wilaya zote za mkoa huo, wenyeviti wa halmashauri, makatibu tawala wa wilaya, wakuu wa taasisi za umma ikiwamo Mamlaka ya Wanyamapori (TAWA) na Wakala wa Huduma za Misitu (TFS), kamati za ulinzi na usalama za wilaya na wakurugenzi kutoka Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Baadhi ya mawaziri walioambatana na Waziri Mkuu ni pamoja na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Anjela Kairuki; Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki; Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete na Naibu Waziri wa Kilimo, Antony Mavunde.

MZALENDO UK 3



# Majaliwa ataka udhibiti wa mifugo wilayani

Na MWANDISHI WETU

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amewaagiza Wakuu wa Wilaya kuitisha vikao na wafugaji kujadiliana na kuweka namna bora ya kufanya shughuli za ufugaji,ikiwa ni pamoja na kutambua mifugo yote iliyoko ndani ya wilaya husika na kuweka zuio la mifugo mingine kuingizwa.

Pia, Majaliwa ameagiza viongozi katika mikoa na wilaya kuweka mpango wa matumizi bora ya ardhi katika maeneo yote yenye wafugaji na wakulima katika vyanzo vya maji.

Majaliwa aliyasema hayo jana wakati akiongoza kikao cha pamoja na Mawaziri wa Kisekta, Makatibu na Naibu Makatibu wakuu, Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoa na Wilaya za Morogoro wadau na wasimamizi wa masuala ya ardhi na mifugo kutatua, changamoto za usimamizi wa masuala ya ardhi ndani ya mkoa huo.

Kikao hicho kimefuatia maagizo ya Rais Dk.Samia aliyoyatoa Desemba 22, mwaka huu,wakati akifunga njia ya kuchepusha maji na kuanza ujazaji maji katka Bwawa la kuzalisha umeme la Julius Nyerere (JNHPP).

"Agizo la Rais ni lazima litekelezwe kwa sisi wasaidizi kutimiza wajibu wetu na kuweka mikakati ya kutekeleza agizo hilo kwa ufanisi,"alisema.

Katika hatua nyingine, Majaliwa aliwataka wakuu wa Wilaya kuunda kamati za maridhiano baina ya wafugaji na wakulima, kutengeneza umoja kati ya makundi hayo mawili kwa kuwataka wawashirikishe wafugaji kuandaa miundombinu ambayo wanyama wao wataitumia kupata malisho, maji na majosho.

Pia alikemea vitendo vya rushwa kuanzia katika ngazi ya viongozi wa Serikali za vijiji, "Unakuta kiongozi wa kijiji anaruhusu wafugaji kutoka maeneo mbalimbali, kwa sababu tu amepewa rushwa na anasahau athari ambazo wanazipata wanavijiji wao.

"Jambo lingine muhimu tutambue maeneo yote ya vyanzo vya maji, pamoja na kutambua maeneo ambayo ng'ombe wanaingia katika maeneo ya vyanzo vya maji na kuwaondoa wote ili maji yaendelee kutiririka kuelekea katika bwawa la umeme,' alieleza.

Vilevile Majaliwa alikubaliana na maombi ya Mkuu wa Mkoa wa Morogoro la kuwaondoa wafugaji walioko katika eneo la Mto Kilombero, ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Rais Dk.Samia.

### RC FATUMA MWASA

Awali,akizungumza katika kikao hicho Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Fatma Mwasa, alisema hali ya usimamizi wa ardhi na vyanzo vya maji katika mkoa huo siyo ya kuridhisha, kwani maeneo mengi ya vyanzo vya maji yameathirika hivyo zinahitajika jitihada za haraka kunusuru hali hiyo.

"Maeneo ya madakio ya maji ya Mto Kilombero hadi sasa yameathirika kwa asilimia 80 na asilimia 20 iliyobaki ndio inayotegemewa kuzalisha maji katika mto huo, tusipochukua hatua sasa hali itakuwa mbaya zaidi.

CamScanner

...mevigawa kwa wanawake

# Maelfu vifaranga vya kuku vyazuiwa Airport

**Na MWANDISHI WETU**

SERIKALI imezuia vifaranga 62,730 vya kuku wa mayai kuingia nchini, baada ya kubainika kutokuwa na vibali na cheti cha afya.

Taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Profesa Hezron Nonga, ilisema vifaranga hivyo ni mali ya Kampuni ya Phoenix Farm Limited ya Mkuranga, mkoani Pwani.

Vifaranga hivyo vilivyokuwa vikitokea nchini Ubelgiji na kuzuiwa katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) eneo la mzigo; vilikuwa vimehifadhiwa katika makasha 697 na vinaonesha kugharimu zaidi ya sh. milioni 200.2.

"Mkurugenzi wa kampuni na wakala wa mmiliki wa vifaranga hivyo walikiri kutokuwa na kibali, hivyo amevunja sheria ya magonjwa ya wanyama Sura ya 156 na Kanuni za Udhibiti wa Usafirishaji wa Wanyama na mazao yake.

"Kanuni ya 26 ya Kanuni za Udhibiti wa Usafirishaji wa Wanyama na Mazao yake ya mwaka 2007 inabainisha, ikiwa wanyama au mazao ya wanyama yatafika nchini bila kibali na cheti cha afya ya wanyama au mazao ya wanyama, mkaguzi aliyeko kituo cha ukaguzi azuie uingizaji wa wanyama au mazao ya wanyama husika nchini," alifafanua.

Alisema vifaranga hivyo vimezuiwa kuingia kwa sababu ni mzigo hatarishi, hivyo Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeutaka uongozi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) tawi la Uwanja wa Ndege Dar es Salaam, kuielekeza Kampuni ya Phoenix Farms Limited kuvirudisha nchini Ubelgiji kwa sababu vinaweza kuhatarisha usalama wa kuku nchini.

> **Mkurugenzi wa kampuni na wakala wa mmiliki wa vifaranga hivyo walikiri kutokuwa na kibali, hivyo amevunja sheria ya magonjwa ya wanyama Sura ya 156 na Kanuni za Udhibiti wa Usafirishaji wa Wanyama na mazao yake.**
>
> Profesa Hezron Nonga

Pia, amemtaka Mkurugenzi wa Kampuni ya Kampuni ya Phoenix Farms Limited, kuviondoa vifaranga hivyo katika maeneo ya uwanja wa ndege na kuvirudisha alikovitoa.

Mwaka 2006 Tanzania iliweka zuio la uingizaji wa kuku na mazao yake kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa mafua makali ya ndege duniani (HPAI).

Mkurugenzi huyo alisema kutokana na zuio hilo, nchi imeendelea kuwa salama dhidi ya ugonjwa huo ambao umeathiri nchi nyingi duniani.

Ugonjwa wa mafua makali ya ndege huambukiza wanyama na binadamu na hutokea kwa njia ya mlipuko na kusababisha madhara makubwa ikiwemo vifo vingi vya kuku na ndege wa porini.

Njia za kudhibiti ugonjwa huo ni kuzingatia usafi katika mabanda ya kuku na karantini ya kuzuia kuingiza kuku, ndege wengine na mazao yao.

Pia, aliwataka Watanzania na wadau wa kuku kuzingatia sheria, kanuni na miongozo iliyopo ya kudhibiti kuingia na kuenea magonjwa ya kuku nchini kulinda usalama wa kuku, ndege wengine na afya ya jamii ya wananchi kwa ujumla.

